# HASIRA HASARA

**Igizo**

Mwanawetu Mmuni

# HASIRA NI HASARA

Hakimiliki © Mwanawetu Mmuni

P.O BOX 90, MTWARA – TANZANIA

Email; Mwanammuni@gmail.com

ISBN 978- 1387-10808-4

© 2017

**MWANAWETU MMUNI**

# YALIYOMO

HASIRA NI HASARA ........ 2
UTANGULIZI ........ 4
SURA YA KWANZA ........ 6
Ushirikiano ........ 6
Mawindo ........ 10
SURA YA PILI ........ 15
Nyumbani kwa Ngao shida imetokea ........ 15
Nje ya zahanati ........ 23
Uaminifu ........ 23
SURA YA TATU ........ 26
Utengano ........ 26
Ni huyu huyu! ........ 31
SURA YA NNE ........ 42
Nguvu za dola ........ 42
Majuto ni mjukuu ........ 46

## UTANGULIZI

Wawindaji wanne walikuwa wanashirikiana kufanyakazi na kila walichokipata waligawana sawa sawa. Walitumia vifaa vya asili kuwinda wanyama, walifanikiwa kwa kuwa waliishi katika kijiji kilichopo pembezoni mwa msitu mnene wenye kusheheni miti mirefu na wanyama mbalimbali hadi baadhi yao kuwa kero wanapofanya usumbufu kwa wakulima pindi wanaposhambulia na kuharibifu mazao yao.

Tatizo la wananchi kujichukulia sheria mkononi na kuwahukumu Raia wenzao wakiamini ni wakosaji; kunasababisha kuwadhuru watu wengine wasio na hatia. Ni jambo la kheri kutoa taarifa za matukio mabaya sehemu husika na kuviachia vyombo vya usalama ili kujiridhisha na kumbaini mharifu halisi.

***WAHUSIKA;***

1. Mzee Ngao
2. Mzee Mundu
3. Kibe
4. Madharau (Rau)

   ***Wengine***

5. Mama Kilian (Kili)
6. Kilian
7. Dada
8. Daktari
9. Muuguzi
10. Polisi 1
11. Polisi 2
12. Vijana msituni
13. Mwenyekiti
14. Raia

# SURA YA KWANZA

## Ushirikiano

ONESHO LA 1

Wanaonekana wawindaji wanne wapo nje ya nyumba (kibanda) chini ya mti wanachonga vijiti na kusokota kamba, kupiga chelea panga, mikuki na kujaribu kulenga shabaha na kuvichoma vitu mbalimbali vilivyokaribu kwa kutumia mikuki na mishale. Mavazi yao ni chakavu, Kibe anavuta sigara…..! wanaonekana wenye furaha na matumaini.

ONESHO LA 2

Wanaonekana wapo msituni, wamebeba silaha na mitego ya wanyama. Mbele katangulia Rau, anakatakata matawi ya miti midogo midogo kando ya njia;

**MUNDU**; Mmh! Rau upo kama mtoto, kazi gani hiyo unayoianzisha?

*Wote wakacheka.*

**NGAO**; Hajamaliza michezo!

**RAU**; Ah! dhihaka hiyo. Mimi ninafamilia halafu mnaniambia bado nacheza? Hapa ninajaribu kama chuma kimekubali chelea? "aliongea kwa tabasamu pana, kuonesha ameelewa wenzake wanamtania."

**NGAO**; Chuma kipo vizuri hicho!

**KIBE**; Eeh! Rau kwa chelea, mtaalamu. Kesho na mimi unisugulie panga langu, “aliongea akiwa anajaribu kushika makali ya panga kwa kiganja cha mkono.”

**MUNDU**; Haya tayari umeshapata wateja, basi na mimi….!

*Wote wakacheka na safari ya kutokomea msituni ikaendelea.*

*(Maongezi yakakatishwa walipozuiwa na Kibe ghafla;)*

**KIBE**; Subirini kwanza…..! “alinong’ona”

*(Mbele bado yupo Rau anafuatwa na Kibe halafu Ngao na mwisho Mundu.)*

Anaonekana Kibe amesimama na walionyuma yake wote wakasimama pia.

Rau akaguswa kwa kutumia mti alioushika kwenye mkono wa kushoto sababu mwingine ulishikia upanga nae akasimama.

*Ilisikika sauti kama kuna mnyama anatembea kwa hatua za taratibu lakini sauti ilikoma baada ya wao kukaa kimya kwa muda.*

*Mzee Mundu akatoa ishara ya kichwa na mikono bila kutoa neno, kuamrisha waendelee kutembea.*

Wanaonekana wanatembea kimya kimya huku wakipiga jicho huku na huko hadi wakafika sehemu iliyowazi baada ya miti mingi mikubwa kukatwa na kuachwa matawi madogo madogo wakati mashina na vipande vingine vikikosekana. Matanuru ya

mkaa, nyasi ndefu zilizolazwa chini, na uharibifu mwingine wa mazingira!

*Ingawa wawindaji wanaonekana lakini hayakusikika mazungumzo yao bali kuonekana wanatikisa vichwa kuashiria kuwa kile wanachokiona ni uharibifu unaofanywa na binadamu wenzao.*

**Mawindo**

ONESHO LA 3

*Baada ya kupita eneo lililoathiriwa na uvunaji haramu wa mazao ya misitu, Rau akamuona mnyama kwa mbali. Akasimama na kuwaonesha wenzake*.

Wanaonekana kila mmoja amechukua nafasi upande wake, wanawasiliana kwa ishara

pekee. Rau ndiye aliyekaa vizuri kwa mashambulizi baada ya kufanikiwa kusogelea windo. Kwa ufundi zaidi akavuta wavu wa upinde na kuachia mshale. Ukaenda kutua kwenye kiuno cha mnyama! Akajaribu kutembea lakini akashindwa na kudondoka chini.

Wakati huo wawindaji wengine pia wapo tayari kurusha mishale, hivyo wakalegeza kamba na kutoka mafichoni kuelekea lilipodondokea windo lao. Haikujulikana nani aliyeachia uzi na kuua mnyama, wakagundua ni Rau ndiye aliyekamilisha adhima ile sababu amebakiwa na mshale mmoja na alichukua miwili.

**MUNDU**; Bwana mdogo upo vizuri, " aliongea akimpiga piga mabegani" …..na mimi

nilishaanza kuachia mkono, ghafla naona mzigo unagaa gaa nikasema, ‘wohi!’ Mashujaa wangu wameniwakilisha vema.

**KIBE** na **NGAO**; Hongera Rau, hongera kijana!

**RAU**; Asanteni (alijibu akicheka), niliwaambia mimi sio mtoto.

**NGAO**; Bado unayo? Pole baba, tumeamini wewe ni jembe.

*Wakacheka!*

ONESHO LA 4

*Wanaonekana wamepata mnyama mwingine*.

Jioni, jua linazama; Rau na Kibe wanaonekana wamebeba nyama nyingi. Wametumia kufunga miguu ya wanyama na

kuning'iniza kwenye kipande cha mti. Mzee ngao na Mundu wamebeba digididigi na pakacha lenye Kanga. Wanaonekana kutembea hadi wanazama na kuonekana tena wapo nyumbani kwa Mzee Ngao. Wanachukua kitoweo kiasi kidogo kila mmoja kwenye chombo chake na nyama nyingine nyingi ikabaki ikiwa vipande vipande. Mzee Mundu akahesabu vipande hivyo na kuangaliana kuashiria kuridhika kwa kile kilichopatikana.

*Giza ilishaingia, wakaagana;*

**MUNDU**; Kesho bwana, ngoja sisi tukawakute watoto. Tunashukuru leo tumefanikiwa kupata windo mchana kweupee…! *ng'ombe anakula majani*. Basi -acha- niwahi.

**NGAO**; Sawa, ninyi nendeni.

**KIBE**; Jioni njema bwana! Utamwambia Mama Kili, tumeshaondoka! (Mke wa Mzee Ngao)

**RAU**; Haya nilikuwepo! "akainuka taratibu kwa uchovu"

**NGAO**; Karibuni tena! ngoja niwahudumie wateja. Jamani eeh, vipi kuhusu kesho?

**MUNDU**; La kesho ni kesho hiyo hiyo!

**NGAO**; Sawa

**MIDUNDO/MUZIKI**

# SURA YA PILI

## Nyumbani kwa Ngao shida imetokea

ONESHO LA 5

Wanaonekana wawindaji wapo nyumbani kwa Ngao sehemu wanayoitumia kutengenezea vifaa vya kuwindia; Wana huzuni, wengine wamekaa na mmoja amesimama kaegemea mwembe, mkononi kashikilia fimbo anayoitumia kuchimba chimba aridhini.

**MUNDU**; Yaani hapo umetuchanganya sana! kwanini utumie fedha zetu bila kutushirikisha? "aliongea kwa hasira"

**KIBE**; Wewe nenda katupatie fedha zetu hayo mambo ya dharula zako, sisi hazituhusu. Kila mmoja anashida zake nyingi sana ……!

Kama zisingalikuwepo fedha hizo, hayo matatizo yako ungalitumia fedha zipi kutatulia? Mimi sikuelewi, nataka changu! "aliropoka maneno bila ya kumtazama sura"

**NGAO**; Jamani….!

**KIBE**; Wewe Mzee usitie neno …. cha … msingi, kaleta pesa tu basi! "alimkata kauli."

**RAU**; Kwani ilikuwaje? Ujue mimi sielewi.

**MUNDU**; Wewe usichoelewa ni nini? Fedha zikitafunwa na wanaojiita wajanja wewe hujui? Umeshadhurumiwa hivyo!

**RAU**; Aaaah….!

**KIBE**; Tuondokeni lakini jioni tukute fedha yetu taslim, sio longolongo tena.

**NGAO**; Nitawatafutia. Sina nia yakuwadhurumu, tuwiane radhi jamani, "aliongea kwa simanzi…. akiwa anafikicha viganja vyake vya mikono."

*(Mundu na Kibe wakaondoka na kubaki Rau na Ngao)*

**RAU**; Naomba nifafanulie, ilikuwaje hadi ukatumia fedha za wenzako? Jana usiku hadi leo, tayari umeshapata majanga na ukatatua kwa fedha hizo hizo za watu. Hakuna michongo mingine ya kujiongeza? Huna akiba? Ona sasa, Wenzetu wameshakasirika. Kibe mwanae karudishwa toka shuleni, ana barua ndefu ya michango halafu wanakaribia kufanya mitihani. Hivi pale amekasirika kweli sio utani.

**NGAO**; Michango gani tena na siku hizi elimu bure? Sio kusudio langu na nitalipa zote! Naombeni mnielewe.

**RAU**; Anasoma VETA, wanalipa! "alijibu kwa mkato na hasira kidogo. Ngao aligundua hali hiyo."

**NGAO**; Jana ilikuwa hivi;

ONESHO LA 6

Anaonekana mke wa Ngao (Mama Kili) anagaa gaa kitandani … mara chini mara juu ya kitandani …. Anatoka nje na kurudi ndani mara kwa mara mwishowe Ngao akatoka nje mbio na ghafla akarudi akiwa ameambatana na mwanamke mmoja kisha wakaingia ndani kwa pamoja, nusra wavunje mlango. Wakamkuta mgonjwa amening'iniza

kichwa chini uvunguni mwakitanda, mkono mmoja upo juu ya stuli. *Inaonesha alikuwa anataka kuchukua kikombe cha maji ya kunywa kilichopo juu yake, lakini alipoteza fahamu kabla ya kukifikia*.

Ngao akamrukia mke wake na kumhifadhi vizuri kitandani, dada wa mkewe (shemeji yake) kapigwa na bumbuwazi na kushindwa kufanya lolote. Ngao akatoa nje baiskeli yake haraka na kuingia chumbani kumbeba magonjwa. Akamwambia shemeji yake;

**NGAO**; Twende! Twende! Njoo umshike. Mwamshe Kili aje kufunga mlango.

*Wakatoka nje mbio na mlango ukafungwa, lakini ghafla!*

**NGAO**; Usifunge kwanza, "mgonjwa alimlaza chini."

*Akasukuma mlango na kuingia ndani kuchukua mfuko wa plastiki ulio chini ya mkeka 'mchagoni' na kumpa shemeji yake*

**NGAO**: Weka kwenye, mkoba "alisema."

*Akamwinua mke wake na kumkalisha juu ya baiskeli halafu kiwiliwili akakiegesha kifuani na kichwa akakiweka mabegani ndipo safari ya kwenda zahanati ikaanza. Mke wa Ngao ni mjamzito.*

ONESHO LA 7

Wanaonekana wameshafika zahanati, mama Kili 'amezinduka' ingawa bado anaendelea na matibabu kwakuwa hata

maji aliyotundikiwa hayajaisha kwenye chupa;

**NGAO**; Pole sana mke wangu, nashukuru upo mzima. Kweli Mungu ni mwema.

*Mara anaingia dada yake amebeba beseni la chuma mkononi alilotumia mgonjwa wao kuwekea uchafu.*

**DADA**; Eeh ameamka! "Alizuia midomo kwa kiganja baada ya kuweka beseni chini kwa haraka tena sehemu isiyo rasmi kisha kuinua juu kutoa shukrani kwa Muumba wake."

ONESHO LA 8

Wanaonekana Daktari na Muuguzi wanaingia kwenye chumba cha mgonjwa na kuwataka Ngao na shemeji yake watoke

nje ili wabaki na mgonjwa kwa uchunguzi zaidi;

**DAKTARI**; Naona mgonjwa anaendelea vizuri, sasa ninyi nendeni kwanza nje ili tumpime ingawa msiende mbali au abaki mmoja ili kukiwa na lolote tuweze kumpa taarifa. Lakini yuko vizuri, sasahivi hakuna haja ya kwenda kituo cha afya. Ondoa shaka Mzee, "alimshika bega Mzee Ngao."

**NGAO**; Asante Daktari, haya sisi tuko nje hapo.

*Ingawa Mama Kili ni mjamzito mwenye mimba pevu, anatakiwa kulipia kiasi cha gharama za matibabu kwasababu alikuwa hajaanza kuhudhuria kliniki ya mama na mtoto.*

**Nje ya zahanati**

ONESHO LA 9

**NGAO**; Sasa wewe baki hapa usitoke. Ngoja mimi nikaangalie nyumbani, si unajua tulivyoacha? Pia nikawajulishe wenzetu kinachoendelea. Nimeshalipia gharama zote, shika hii labda kutakuwa na lolote la haraka "alimpa fedha kidogo."

**Uaminifu**

ONESHO LA 10

Nyumbani kwa Ngao;

**RAU**; Mgonjwa anaendeleaje sasa?

**NGAO**; Hajambo lakini mimi sijakwenda tena nilikuwa ninawasubiri ninyi ili niwaambie kuwa fedha zenu nimezikopa. Nimemtuma Kili

kupeleka staftahi. ingawa nimeongea nae kwa simu, nashukuru hajambo lakini bado hawezi kutembea.

**RAU**; Pole sana! ungeliwaambia vizuri, wangelikuelewa, "aliongea kwa huzuni."

**NGAO**; Muda gani? Watu hawajataka kunipa nafasi ya kujieleza.

**RAU**; Mmh pole, haya bwana nitakukuta baadae tukamuone mgonjwa, unatarajia kwenda saa ngapi?

**NGAO**; Nakwenda sasahivi, utanikuta huko huko! Ukifika tu, utaniona. Amepumzishwa kwenye jengo la kwanza huku, "anaonesha kwa mikono sambamba na kuchora chini ramani ya jengo lilipo." …..Au nipigie simu kama hautaniona nje.

**RAU**; Sawa.

***

*MIDUNDO/MUZIKI*

# SURA YA TATU

## Utengano

ONESHO LA 11

*Baada ya wiki moja yenye mgogoro kupita; Kibe, Rau na Mundu wakaenda porini kuwinda peke yao, hawakutaka ushirikiano na Ngao*.

Wanaonekana wapo porini na wamefanikiwa kupata nyama nyingi. Sura zao zimenawili kwa furaha na vicheko. Wakiwa wamekaa chini wanajiandaa kufunga nyama vizuri tayari muda wa kurejea nyumbani.

*Wanaanza kutoka tu! Kibe na Rau wamebeba nyama kama kawaida Mundu amebeba pakacha lenye ndege*

*anayeonekana miguu inayofanana na Kanga au kuku pori 'kereng'ende'kama wenyeji wanavyomuita;*

**ONESHO LA 12**

Ghafla wanaonekana wamevamiwa na watu wawili waliovaa nguo zinazofunika kichwa kizima na kuacha upenyo wa macho tu. Kwa kuwa ilikuwa haraka, Rau na Kibe wakaanguka chini pwaa! Wakifuatiwa na windo lao juu. Kila kitu kikadondoka kimoja huko na kingine kule yaani silaha zao nazo zikawaponyoka!

*Kuona lile varangati, Mundu akachukua muda huo kutoroka na kwenda kujificha kichakani.*

Anaonekana kubadilisha vichaka; Kichaka cha kwanza akaona ki-angavu sana hivyo anaweza kuonekana na kuanza kukifuata kichaka kingine.

*Kubabaika ili wasimwone wadharimu hao wa roho za watu kukazua balaa jingine;*

Anaonekana Mundu anajichoma mti usoni na kuanza kuvuja damu. *Maumivu yakamsahaulisha kama yupo mafichoni na kuanza kupiga yowe*.

**MUNDU**; Mama wee! Nafwa! "Mara akili ikamrejea na kukumbuka yupo kwenye harakati za kuokoa roho yake inayokaribia kutoweka, akakatisha kilio kama mwanga gizani. Kisha akajikokota kwenda kwenye

kichaka kilichokaribu yake na kujibwaga chini machozi yakimtiririka."

ONESHO LA 13

Wakati huo huo

Kibe na Rau wanaonekana bado wanaendelea kupokea kichapo, kila wanapojaribu kujitetea ili wakimbie, wanashindwa! Sababu wanapigwa mitama, mateke na ngumi nzito hadi wavamizi wanaonekana kushinda kupora nyama. Mvamizi mmoja akawa anaendelea kutembeza kipigo na mwenzake akabeba nyama na kutokomea nayo msituni.

Kibe amekunjwa kisawa sawa ndipo Rau akapata upenyo wa kuinuka na kupata wazo la kumkimbilia anayepora nyama.

Anaonekana kumkaribia, nae mwizi akamuona pia. Kumbe wameshafika mahali walipodondoka kwa mara ya kwanza. Yule mvamizi bila hajizi anaonekana kuokota mkuki mmoja na kumchoma nao Rau tumboni!

*Rau akaushika mkuki ule kana kwamba anataka kuuchomoa na mwishowe akadondoka chini. Maskini! Kumbe mikuki na mishale wanayoitumia, wanaipaka sumu ili mnyama akichomwa, afe haraka ili asiweze tena kukimbia.*

*Kibe akaona Rau amejeruhiwa, akapiga ukunga;*

**KIBE**; Mayooo! Rau usiniache mwenzio! Nitakwenda kusema nini nyumbani? Nani

ataniamini mimi? Njoo uniue tu na mimi! "akalia sana bila msaada."

*Mwizi akatumia mwanya huo kutorokea msituni kumfuata mwenzake.*

**Nyumbani kwa Ngao**

ONESHO LA 14

**Ni huyu huyu!**

Wanaonekana Mundu na Kibe wanapiga hodi kwa Ngao wakiwa vile vile na nguo zao chafu, ngeu na hasira walizotoka nazo kwenye mpambano kati yao na madharimu. Ngao anaonekana anatoka nje na kuwakaribisha kwa tabasamu la ukarimu baada ya kusikia sauti za swahiba zake na akajisemea;

**NGAO**: Nashukuru leo nitalipa deni, inaonesha wanahasira na fedha yao.

*Akashindwa kutambua kama watu hao wametota damu sababu tayari kuna giza. Bali yeye anayetoka ndani ndiye anayeonekana kupitia mwanga hafifu wa koroboi unaopenya mlangoni. Kibe na Mundu wakasimama kwenye pembe moja ya nyumba hiyo kama vile wanavizia kutaka kujua jambo.*

**MUNDU**; Haya tupe habari, kwanini umetufanyie vile? Rau alikukosea nini? We mbona mnafiki sana! Yule kijana aliungana na wewe kuuguza mkeo juzi tu hapa, na leo unamuua! "aliuliza maswali mengi lakini kwa bahati mbaya wakashindwa kuelewana."

**NGAO**; Kwanza nitawakabidhi mzigo wenu kabla ya asubuhi, hivyo karibuni sana mketi. Tusameheane, yaliyo…..!

**KIBE**; Eeh! unasemaje? "akamkata ulimi."

Anaonekana Kibe anamsogelea Ngao na kumkata mtama, Ngao akadondoka chini kama gunia la pamba. Mundu akapandisha jazba na kuendelea kuongea;

**MUNDU**; Kumbe wewe hautujui vizuri? "Akaingia ndani kwa Ngao na kurejea akiwa amechukua mkuki mmoja"

**MAMA KILI**; Kulikoni? "kashika beseni inaonekana anatoka kupeleka kitu mahali na hasa ilikuwa nyama. Sababu chombo hicho kimenona kwa damu baada ya kuonekana kupitia mwanga hafifu wa tochi inayotumia

betri chakavu zilizotolewa kwenye redio. Tochi ambayo imetumika kuona njia na sasa imemulika damu ya kwenye beseni baada ya kulibwaga chini kwa mshtuko kutokana na hali aliyoikuta nyumbani kwake."

**KIBE**; Unaona! Unaona! Mundu, mimi sikubali Rau apotee hivi hivi!

**NGAO**; Kwani kumetokea nini jamani?

Anaonekana Mama Kili anamshika mume wake na kujaribu kumwinua toka chini alipodondokea baada ya kupigwa ngwala na Kibe. Mundu anainua mkuki juu tayari kumchoma Ngao lakini akashindwa kuushusha juu ya mwili wake kwasababu mama Kili akawahi kazuia kwa mbele.

**KIBE**; Unajua huyu mshenzi ametutesa sana!

*Anaonekana Kibe anaingia ndani ya nyumba ya Ngao kama kifaru;*

**KIBE**; Aaah! "akadondoka chini baada ya kuiona nyama ipo kwenye upambo imebanikwa jikoni na kongoro zimewekwa kwenye ungo. Akakumbuka nyama iliyoporwa msituni, na jinsi Rau alivyodondoka kama mzoga!"

*Akapandwa na hasira na kuchukua panga lililopo chini karibu na jiko ambalo lilitumika kucharanga minofu na kutoka nalo nje kwa kasi ya ajabu hadi kwa Ngao. Akamkuta ameshainuka anajipangusa vumbi mwilini, mama Kili anajitahidi kumsihi Mundu apunguze jazba na awaambie kilichotokea*.

Wanaonekana kukatishwa maongezi yao na ujio wa Kibe kuelekea walipo na bila kupoteza muda, panga likatua kichwani kwa Ngao na kumfyeka kisawasawa! Akadondoka chini na kuanza kububujikwa damu nyingi kama bomba lililopoteza koki.

**KIBE**; Lete mshale nimmalize! Dawa ya moto ni moto!

**MUNDU**; Huyu acha nimmalize mwenyewe, "akamzuia Kibe kuchukua mkuki lakini bila kupoteza muda mkuki ukatua na kukita kwenye kifuani cha Ngao"

**NGAO**; Mama nakufaa! "akalia kwa sauti kubwa ya uchungu."

**MAMA KILI**; Mtumee! Mume wangu! "nae akadondoka nakupoteza fahamu."

**MUNDU**; Kufa tu kama ulivyomuua Rau, mnafiki mkubwa!

*Kifo kikamfika Ngao haraka sababu mkuki uliotumika pia uliwekwa sumu tayari kwa mawindo ya wanyama siku inayofuata.*

*Sauti kali zenye masikitiko walizozitoa zikawavuta majirani na kugundua tofauti nakusema, "huo sio mzozo wao wa kawaida tuliouzoea kwa wiki mzima sasa." Hivyo wakasogea kushuhudia kinachojili, ndipo wakakuta mambo yameshaharibika. Wahenga husema mchelea mwana kulia…..!*

*Ujenzi wa nyumba za wakazi wa kijiji hiki ni mbali mbali sana kwahiyo ni vigumu kutambua mapema mazungumzo ya kheri au shari.*

Wanaonekana Kibe na Mundu wanachanja mbuga na kutoweka baada ya kutamatisha tukio hilo na kuwaona wasamalia wema wanakuja, kuhofia na wao kugeuziwa kibao.

***

ONESHO LA 15

Inaonekana kuna matanga katika nyumba zote mbili yaani kwa Rau na Ngao. Wanaonekana watu wamekusanyika wanaomboleza.

*Nyumbani kwa Rau waombolezaji wanamlaumu Ngao kwa uchu wakipato hadi kupelekea kusababisha kifo cha mpendwa wao na baadhi wakawapongeza Kibe na Mundu kwa ujasiri waliouonesha wa kuhakikisha nae wanamuondoa duniani*

*kutokana na mabaya yake kwa maana ya mshahara wa dhambi ni mauti.*

ONESHO LA 16

*Wakati nyumbani kwa Ngao ambako kulikuwa na watu wachache kwa kuita "msiba wa kujitakia"* mama Kili anaonekana analia peke yake hadi alipofika dada yake pamoja na kifungua mimba wao Kilian.

*Watu hawa majonzi yao ni makubwa wakiamini ndugu yao amedhurumiwa haki yake ya kuishi kwa uonevu.*

ONESHO LA 17

Mama Kili anakumbuka;

Anaonekana Ngao anamsimulia jinsi alivyoagua mtego na kumpata mnyama mkubwa kwa kubahatisha.

**MAMA KILI**; Sasa kwanini wamtuhumu amenyang'anya na kumsababishia kifo cha Rau? Kwa kinywa chake alisema;

**NGAO**; "Alimkumkuta mnyama amenaswa katika mtego wake alioutega jioni ya siku iliyopita" Akanisimulia alivyomfungua na kuleta nyama nyumbani bila kupata usumbufu wowote.

**MAMA KILI**; Halafu alikwenda kuwinda msituni asubuhi na sio jioni kama wasemavyo wao! Sasa niamini lipi? "aliwaza."

Akarudisha mawazo na kuendelea kumlilia mume wake ambaye hatomuona tena ili amfumbulie fumbo hili.

***

*MIDUNDO/MUZIKI*

# SURA YA NNE

## Nguvu za dola

ONESHO LA 18

Mwenyekiti yupo kaunta ya polisi

**MWENYEKITI**; Mimi ni Mwenyekiti wa kijiji cha Lindu, nimekuja kuleta taarifa kuwa katika eneo langu kumetokea tukio la mauaji ya watu wawili.

**POLISI 1**; Eeh! Afande sogea kwanza tumsikilize jamaa huyu amejitambulisha kuwa Mwenyekiti wa kijiji na ameleta taarifa ya kutokea uharifu katika eneo lake. Watu wawili wameuawa.

Anaonekana Askari Polisi mwingine anasogea karibu na kuanza kusikiliza na kuandika maelezo ya Mwenyekiti kwa

umakini mkubwa kabla ya kuambatana nae kwenda eneo la tukio.

ONESHO LA 19

Wanaonekana Wanachukua silaha za moto na kutumia usafiri wa pikipiki kubwa kuwafikisha kijijini. Wakakuta familia zote mbili, zinaendelea na maombolezo.

ONESHO LA 20

Inaonekana maiti zote mbili zinakusanywa eneo moja kisha Polisi mmoja akatoa amri zipimwe haraka na baada ya hapo, zitazikwa.

**POLISI 2**; Waombolezaji poleni sana kwa msiba. Hii hali imeshatokea, ni tabia mbaya kwa raia kujichukulia sheria mkononi na kutoa hukumu iwe kweli kuna kosa linaloonekana

au kuthibitisha ama si kweli. Vitendo kama hivi, havikubaliki. Waliofanya haya ni lazima waingie kwenye mkono wa sheria, wasijidanganye kutoroka. Hawana mahali watakwenda kujificha ambako tutashindwa kupajua na kuwakamata. Kufanya hivyo ni kuliongezea hasira jeshi la polisi.

*Hotuba ikaendelea ikiwa Daktari anaendelea kuchukua vipimo.*

Polisi alizungumza na ndugu wa marehemu;

**POLISI 2**; Daktari akimaliza shughuli zake, mtapewa kibali cha kuhifadhi miili…..kuzika! Taratibu zingine zitafuata. Poleni sana, naomba ushirikiano wenu kuhakikisha wale wote waliohusika kwa namna moja ama nyingine wanatiwa hatiani.

ONESHO LA 21

*Baada ya shughuli za maandalizi ya mazishi kukamilika; Polisi wote wawili, Mwenyekiti na baadhi ya raia kwapamoja walirudi msituni kuendelea na uchunguzi*.

Unaonekana msafara upo njiani wanaangalia huku na kule sambamba na kuonesha kuhuzunika kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira unaoathiri msitu huo, unaosababishwa na shughuli mbalimbali zakibinadamu ikiwemo kilimo cha kuhamahama.

**Majuto ni mjukuu**

ONESHO LA 22

Wanaonekana kutembea umbali mrefu, baadhi yao wameachwa nyuma baada ya mwendo wao kuwa wa taratibu kutokana na uchovu. Wakakuta kati kati ya msitu mnene kuna sehemu ipo wazi. Kwa mbali wanamuona mtu anatembea bila kujistiri nakumuacha baadhi ya viungo kuwa wazi 'tumbo wazi' wakaanza kuwasiliana kwa kutumia ishara hadi wakafika karibu na eneo hilo kisha kulizunguka.

**POLISI 2**; Tulieni hapo hapo! "akawaelekezea bunduki."

Wanaonekana vijana waliokutwa msituni wanataka kukimbia kujiokoa kutiwa nguvuni

lakini waliogopa kupigwa risasi. Hivyo wakasimama na kutii amri. Walifungwa pingu kabla ya kutoa maelezo ya kwanini wapo porini muda huo? na wanafanya shughuli gani? kwa ruhusa ya nani? Pembeni kulikutwa shehena ya mbao, hivyo inaonesha moja kwa moja wanahusika na uharibifu wa mazingira.

ONESHO LA 23

Anaonekana kijana mmoja miongoni mwa raia anaangalia juu kwa wasiwasi kwa kuwa kamuona mtu amejificha mtini. Lakini bahati ikawa yake pale Afisa wa polisi alipofuatilia macho ya kijana huyo aliyechini na kutogundua kitu anachokiangalia. Akaendelea kuwahoji kwa makini wale aliowaweka kizuizini.

*Linaendelea onesho la 22*

**POLISI 2**; Wenzenu wapo wapi?

**KIJANA 1**; (baada ya ukimya, wanaangaliana) ….wamekwenda kufuata mahitaji

**POLISI 2**; Wangapi?

**KIJANA 2**; Watatu

**POLSI 1**; Sema ukweli, Mpo wangapi?

*Wakapata kichapo kidogo sababu walitafuna maneno badala yakujibu ipasavyo.*

ONESHO LA 24

Mwenyekiti na Polisi 2 wanaonekana kuendelea kutalii katika eneo hilo hadi wakagundua kando kuna shimo lenye

vyombo na kuna jungu limefunikwa chakula. *Baada ya Polisi 2 kufunua chungu hicho kikubwa kushuhudia kilichomo, wakakuta ni kongoro. Mwenyekiti akashindwa kujizuia.*

**MWENYEKITI**; Ah! unaona sasa?

Watu wote wakaangalia muelekeo huo, kwa pembeni kuna kibanda uchwara na kuona nguo, mizura iliyotobolewa matundu mfano wa macho, mkuki na vingine vingi.

**POLISI 2**; Mmh! (akiwa na hasira, akamwambia mwenzake) tuchukue na hivyo!

**MWENYEKITI**; (Kwa mnong'ono) ….halafu Mundu alisema' waliowavamia walivaa vibwengo! Oneni mambo haya! "akaanza kulia kwa sauti"

**MWENYEKITI**; Jamani eh! Ngao wa watu ameuawa buree! Kumbe hawa wanaharamu ndiye waliomuua Rau kushibisha matumbo yao…! "*akaomboleza akiwa anapiga piga chini na kujisaga miguu*."

**POLISI 2**; Basi mzee tulia, ni kweli inaumiza sana tabia ya watu kujichukulia sheria mkononi, madhara yake ni haya.

ONESHO LA 25

*Mwenyekiti akiwa anaendelea kulia, akatupa jicho juu ya mti na kuona kitu ghafla kilio kikasitishwa.*

**MWENYEKITI**; Wewe mshenzi! Shuka mwenyewe kabla sijakupopoa kama maembe, ngedere mkubwa wewe!

*Wote wakaangalia juu na kumuona mtu kajificha kwenye tawi la mti.*

**MWENYEKITI**; Nyamafu mkubwa we!

*Kabla hata ajakaribia kufika chini tayari akajikuta kashavaa pingu na kichapo cha kumuondoa 'wenge' kisha kuunganishwa na wenzake.*

Walipomaliza kuwafichua wote sita; wakarudi nao hadi kijijini halafu kuwasafirisha kwenda kwenye uwanja wa haki wakajibu mashauri yao.

ONESHO LA 26

Baada yakufika kijijini; Wanaonekana raia wanapiga kelele, na kuzomea.

*Kwenye matanga, vilio vikasikika zaidi sababu wakajua kuwa; bila ya wale watu kumdhuru Rau, mzee Ngao asingalikufa, Kibe na Mundu wasingeliwekwa kizuizini.*

"Kweli HASIRA NI HASIRA!" walisikika.

*Kibe na Mundu wakafungwa kifungo cha maisha jela ili kutoa fundisho kwa watu wenye tabia kama zao za kuhukumu kabla ya kufika mahakamani. Hivyo kufanya familia nne kubaki yatima kwa kukosa baba.*

*Wapasua mbao 06 nao wakahukumiwa kufungwa jela wengine maisha na wengine*

*miaka zaidi ya 15 kutokana na makosa kutofautiana.*

*Looh! Kweli hasira hasira.*

**MWISHO**